*Kioo cha Lugha, Juz. 23(2), 369-395*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v23i2.3

# Makovu ya Kisaikolojia ya Utumwa katika Jamii za Watanzania: Historia, Masimulizi na Tajiriba

*Jaquiline A. Moshi*[1] *na Titus L. Ombori*[2]

## Ikisiri

Makala hii inachunguza makovu ya kisaikolojia ya utumwa kwa jamii za Kitanzania kwa kutumia masimulizi ya kihistoria, simulizi za kifamilia na urithi wa kitamaduni kama vyanzo vya msingi vya uelewa wa pamoja wa kihistoria. Kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimaudhui, makala data zimechambuliwa kutoka katika maandiko ya kihistoria, nyaraka za makavazi na simulizi za watu binafsi kuhusu utumwa. Vyanzo hivi vilitumiwa kubaini mada kuu zinazojirudia kama vile fadhaa ya kihistoria, urithishaji wa maumivu ya kihisia, udhalilishaji wa utu na ustahimilivu wa kijamii. Makala hii imeongozwa na nadharia tatu ambazo ni Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii, Nadharia ya Kumbukumbu ya Kihistoria na Nadharia ya Fadhaa ya Kizazi. Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa athari za kisaikolojia za utumwa bado zinaendelea kudhihirika katika jamii za Kitanzania kupitia msongo wa mawazo, huzuni ya muda mrefu, hisia za kutengwa kijamii na mkanganyiko wa utambulisho. Hata hivyo, jamii hizi zimeonesha ustahimilivu mkubwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za kukabiliana na hali hiyo, zikiwamo masimulizi ya kimapokeo, imani za kidini, makumbusho na sherehe za kitamaduni kama njia za uponyaji wa pamoja na ujenzi wa utambulisho chanya.

## 1.0 Utangulizi

Historia ya biashara ya utumwa Tanzania Bara imegubikwa na mateso makubwa na makovu yasiyosahaulika kwa binadamu (Rhodes, 2018). Kwa fasili yake pana, dhana ya utumwa inarejelea hali ambayo watu binafsi wanachukuliwa kama mali, wanalazimishwa kufanya kazi, na kunyimwa haki zao za msingi za kibinadamu. Mtumwa ni mtu anayemilikiwa na mtu mwingine, ambaye uhuru na uwezo wake wa kujiamulia hudhibitiwa na mmiliki wake (Sheriff, 1987; Deutsch, 2011; Lovejoy, 2012; Rushohora, 2024; Nyanto na Becker, 2025). Hali hii ilijenga msingi

[1] Profesa Mshiriki, Idara ya Saikolojia ya Elimu na Stadi za Mitaala, Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Barua pepe: jaquiline.moshi@muce.ac.tz

[2] Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Historia, Sayansi ya Siasa na Taaluma ya Maendeleo, Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,Tanzania.
Barua pepe: titus.ombori@udsm.ac.tz

wa mifumo ya unyonyaji wa muda mrefu ambayo iliathiri si tu maisha ya watumwa bali pia vizazi vyao.

Nchini Tanzania, kama ilivyokuwa katika maeneo mengine ya Afrika Mashariki yaliyohusishwa na biashara ya watumwa kupitia Bahari ya Hindi na ile ya Atlantiki, mamilioni ya wanaume, wanawake na watoto walisafirishwa, waliuzwa, na walilazimishwa kustahimili mateso makubwa (Sheriff, 1987; Deutsch, 2011; Lovejoy, 2012). Madhila hayo hayakuwa tu ya kiuchumi bali ya kijamii na kisaikolojia pia huku athari zake zikiendelea kuonekana hadi leo miongoni mwa vizalia vya watu waliochukuliwa utumwani (Alpers, 1975; Sheriff, 1987). Hii inaonesha kuwa utumwa haukuwa tukio la kihistoria lililopita tu, bali ni urithi unaoendelea kuathiri maisha ya sasa.

Watafiti wa hivi karibuni wamebainisha kuwa urithi wa utumwa hauwezi kufutika kwa kukoma kwa biashara hiyo pekee, bali unaendelea kujitokeza kupitia kumbukumbu, mitazamo na hisia za pamoja katika jamii za baada ya utumwa. Becker na wenzake (2023) wanaeleza kuwa mijadala kuhusu vizalia vya watumwa Afrika Mashariki bado inakabiliwa na aibu ya kihistoria na unyanyapaa wa kijamii unaoifanya mada hii kuwa nyeti kimaadili na kihisia. Wanaongeza kuwa vizalia wengi hubeba mzigo wa kihisia na kijamii unaotokana na historia ya unyonyaji, na kwamba kumbukumbu hizo huathiri nafasi yao katika jamii za sasa. Hali hii huathiri pia jinsi wanavyojiona na wanavyojumuishwa katika muktadha wa kitaifa na kijamii.

Vilevile, Nyanto na Becker (2025) wanaonesha kwamba jamii za waliokuwa watumwa zilijenga mikakati ya kijamii ya kustahimili kupitia kuunda makazi na vijiji huru vilivyowapa uwezo wa kujitambua upya. Kupitia juhudi hizo, walitengeneza maana mpya za uhuru, utu na mshikamano, ambazo ziliwasaidia kuondokana na alama za msongo wa kisaikolojia na kujijenga kama watu huru katika mazingira mapya ya kijamii. Mikakati hii ya kijamii ni ushahidi wa ustahimilivu wa kihistoria na uwezo wa jamii kuunda upya utambulisho wao licha ya historia ya ukandamizaji.

Uchambuzi wa kihistoria unaonesha kuwa athari za utumwa hazikuishia katika kipindi cha biashara yenyewe, bali zimeendelea kuathiri mifumo ya kijamii, kitabaka, na mahusiano ya kitamaduni katika kipindi cha baada ya ukombozi wa kisiasa (Nyanto na Becker, 2025). Banshchikova na Ivanchenko (2019) wanafafanua kwamba kumbukumbu za biashara ya watumwa zimeendelea kuunda mivutano isiyoonekana baina ya makundi yaliyowahi kuwa watumwa na waliokuwa wamiliki. Wanaonesha pia kuwa jitihada za kitaifa za kupandikiza uvumilivu na umoja zinalenga kufuta alama hizo za msongo wa kihistoria, ingawa athari zake bado zinajitokeza katika mazungumzo ya uraia na utambulisho wa kijamii. Hii inaonesha kuwa maridhiano ya kihistoria bado ni mchakato unaoendelea. Aidha, Rushohora (2024) anaeleza kwamba kumbukumbu za mapambano dhidi ya utumwa zimeendelea kuwa chemchemi ya utambulisho wa ukombozi miongoni mwa vizalia. Kupitia masimulizi ya kifamilia na mila za kitamaduni, jamii zimeendelea kuhifadhi

historia ya mapambano na mateso, na hivyo, kuimarisha hisia za uthubutu, kujitambua, na ustahimilivu wa kihistoria. Hii ni ishara ya nguvu ya kumbukumbu kama chombo cha uponyaji na ujenzi wa utambulisho wa pamoja.

Kwa kuzingatia muktadha wa tafiti zilizotangulia, makala hii inalenga kuchunguza makovu ya kisaikolojia yaliyoachwa na utumwa kwa vizalia vya Tanzania Bara, pamoja na namna athari hizo zinavyojitokeza katika utambulisho wa mtu binafsi na wa kijamii. Utafiti huu unatumia mtazamo wa taaluma mtambuka unaojumuisha historia, saikolojia na tafsiri za kitamaduni ili kufafanua jinsi kumbukumbu za utumwa zinavyohifadhiwa, zinavyoathiri ustawi wa akili na jinsi jamii zinavyounda mikakati ya uponyaji na maridhiano ya kihistoria. Kwa kuzingatia muktadha huo wa kihistoria na kijamii, makala hii inatumia mbinu mahuluti inayochanganya vyanzo vya kihistoria, masimulizi ya kifamilia na tafsiri za kifasihi. Mbinu hii hutoa mwanga mpana na wa kina kuhusu namna kumbukumbu za utumwa zinavyoendelea kuathiri nafsi ya mtu binafsi, tabia za kijamii na afya ya kisaikolojia ya vizalia katika Tanzania ya sasa.

Taarifa za utafiti zilikusanywa kupitia mapitio ya maandiko ya kihistoria, makala za kitaaluma na nyaraka za makavazi zinazohusu historia ya utumwa nchini Tanzania. Maandiko muhimu yaliyopitiwa ni pamoja na kazi za wanahistoria mashuhuri kama Abdul Sheriff (1987) na Edward Alpers (1975), sambamba na hati za serikali na nyaraka za kikoloni (URT, 1977). Aidha, masimulizi ya kihistoria yaliyohifadhiwa na simulizi za karibuni zinazohusu vizalia vya watumwa na watu waliowahi kuchukuliwa utumwani yalichambuliwa ili kupata taarifa za kina kuhusu athari za kisaikolojia, kijamii na kiutambulisho wa utumwa.

Uchanganuzi wa data katika utafiti huu ulifanyika kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa kimada, ambayo ilitoa fursa ya kubaini mada kuu zinazojirudia kama vile utambulisho, kumbukumbu, fadhaa na ustahimilivu wa kihistoria. Vilevile, nadharia za Utambulisho wa Kijamii, Kumbukumbu ya Kihistoria na Fadhaa ya Kizazi zilitumika kama miwani ya kinadharia kueleza jinsi uzoefu wa kihistoria wa utumwa unavyoendelea kuathiri tabia, afya ya akili na mienendo ya kijamii ya vizalia vya watumwa katika Tanzania ya sasa. Kwa kutumia maarifa ya kidhahania na mtazamo wa kihistoria, makala hii inalenga kutoa uelewa wa kina na wa kijumla kuhusu makovu ya kisaikolojia ya utumwa, kwa kutambua mwingiliano wa masuala ya kihistoria na ya sasa unaochangia athari za muda mrefu za kiwewe na mabadiliko ya kijamii katika jamii za Tanzania.

## 2.0 Utumwa katika Jamii za Watanzania

Utumwa una historia ndefu katika Afrika Mashariki, ukiwa na sura mbalimbali zilizojitokeza katika jamii nyingi za Kiafrika hata kabla ya kuwasili kwa wafanyabiashara wa Kiarabu na Ulaya (Sheriff, 1987). Hata hivyo, kiwango cha ukatili na mawanda ya biashara ya utumwa viliongezeka kwa kiasi kikubwa wakati wa biashara ya Bahari ya Hindi na ile ya Atlantiki, hali iliyofanya maeneo ya Tanzania kuwa kitovu kikuu cha utekaji na uuzaji wa watumwa (Sheriff, 1987;

Deutsch, 2011). Miji ya pwani kama Bagamoyo, Kilwa na Zanzibar iligeuka kuwa vituo vikuu vya biashara hiyo, ambako mamilioni ya watu kutoka bara walitekwa, waliuzwa, na kusafirishwa kwenda mashambani au masoko ya nje (Alpers, 1975; Sheriff, 1987). Biashara hii iliunganishwa na mitandao ya kimataifa ya utumwa iliyolenga kukidhi mahitaji ya nguvukazi katika Mashariki ya Kati, India na Ulaya (Sunseri, 2002; Lovejoy, 2012).

Njia za kupata watumwa zilihusisha ukatili mkubwa kwa sababu makundi yenye silaha yalivamia vijiji vya bara na kuwakamata wanaume, wanawake na watoto (URT, 1977). Mateka hao walisafirishwa kwa miguu hadi masoko ya watumwa ya pwani, wakikumbana na safari ndefu iliyojaa mateso. Utekaji huu wa kikatili, kushuhudia mateso na kuuzwa na kununuliwa kama bidhaa viliathiri sana afya ya kisaikolojia ya watu binafsi na jamii kwa ujumla (Alpers, 1975). Simulizi kutoka maeneo kama Tabora na Kigoma bado zinabeba kumbukumbu za hofu na uharibifu uliosababishwa na uvamizi huo na, hivyo, kuacha makovu ya kudumu katika fikra za pamoja za jamii (Nyanto, 2019; Deutsch, 2011).

Inakadiriwa kuwa kati ya karne ya 16 hadi 19, zaidi ya Waafrika milioni 28 walitekwa kutoka maeneo mbalimbali ya bara (Lovejoy, 2012). Wengi wao walilazimishwa kutembea kwa miguu hadi pwani wakiwa wamefungwa kwa minyororo, wakikumbana na njaa, ukatili na unyanyasaji (Alpers, 1975). Takribani nusu yao walifariki njiani kutokana na mateso hayo (Curtin, 1969). Aidha, tafiti zinaonesha kuwa wanawake walikumbwa na madhila ya kipekee, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia na unyonyaji wa kazi, huku thamani yao ikibadilika kulingana na umri na uwezo wa uzazi (Wright, 1993; Deutsch, 2007 Wright, 1993).

Kati ya watumwa milioni 14 waliowasili pwani, ni theluthi mbili tu waliweza kuhimili safari ya baharini kupitia Atlantiki, safari iliyodumu kati ya mwezi mmoja hadi mitatu kwa kutumia meli zisizo salama (Lovejoy, 2012). Wengi walikufa kutokana na magonjwa, njaa au walijitoa uhai kutokana na mateso makali (Curtin, 1969). Walionusurika waliuzwa katika maeneo ya Amerika na Karibiani ambako walikumbana na ukatili mwingine mkubwa, hali iliyosababisha vifo vingi kutokana na kazi ngumu, magonjwa na unyanyasaji (Heywood, 2003).

Nchini Tanzania, ingawa wengi walichukuliwa kupelekwa nje ya nchi, sehemu kubwa ya watumwa walibaki kufanya kazi katika mashamba makubwa ya miwa na karafuu huko Unguja, Pemba na maeneo mengine ya bara. Hali ya maisha ya watumwa hawa ilikuwa ya dhiki, wakifanya kazi katika mazingira magumu na mara nyingi wakikumbwa na adhabu kali na udhalilishaji. Hali hii ilisababisha si tu majeraha ya kimwili bali makovu ya kisaikolojia pia, kwani walinyimwa uhuru na utambulisho wao wa kibinadamu (Sheriff, 1987; Deutsch, 1998). Madhila haya yaliacha athari za kudumu katika jamii, ambazo hadi leo zinaendelea kudhihirika kupitia mifumo ya kitabaka, kutengwa kijamii na kiuchumi pamoja na kumbukumbu za pamoja za kihistoria (Nyanto, 2019; Deutsch, 2011; Nyanto na Becker, 2025).

Licha ya juhudi za ukombozi wa watumwa zilizofanywa na wakoloni wa Kijerumani na wamisionari, tafiti zinaonesha kuwa mchakato wa kuwaweka huru

watumwa haukuwa wa huruma wala wa haraka. Mara nyingi, waliokombolewa walikumbana na hali ngumu ya maisha, unyanyapaa na kutengwa kijamii (Deutsch, 1998; Sunseri, 2002). Hali hii ilichangia kuendeleza athari za kisaikolojia na kijamii kwa vizalia vya watumwa hata baada ya ukombozi rasmi.

Mbali na maendeleo ya tafiti kuhusu historia ya utumwa na athari zake kuvutia uangalizi wa kina wa kitaaluma (tazama, kwa mfano, Deutsch, 2011; Mapunda, 2017; Becker, 2021; ; Mikidady, 2023; Becker na wenzake), bado kuna upungufu katika kuelewa kwa kina athari za kisaikolojia za utumwa, hasa katika muktadha wa Tanzania ya sasa. Utafiti mwingi umelenga zaidi vipengele vya kihistoria na kijamii, huku masuala ya kiakili na kiutambulisho yakipewa uzito mdogo. Makala hii inalenga kuziba pengo hilo kwa kuchunguza kwa undani jinsi matukio ya kikatili ya utumwa yalivyoacha athari za muda mrefu katika maisha ya vizalia vya watumwa kwa kuangazia namna kumbukumbu za kihistoria zinavyoathiri ustawi wa akili, mitazamo ya kijamii na ujenzi wa utambulisho wa mtu binafsi na jamii kwa ujumla.

## 3.0 Uundaji wa Utambulisho na Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii

Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii, iliyoasisiwa na Henri Tajfel na John Turner mwaka 1979, inatoa msingi muhimu wa kuelewa jinsi historia ya utumwa ilivyoathiri uundaji wa utambulisho wa kijamii katika jamii za baada ya utumwa, kama ilivyo Tanzania. Kwa mujibu wa nadharia hii, watu hujielewa na kujitambulisha kupitia uanachama wao katika makundi ya kijamii, ambapo tofauti baina ya "sisi" na "wao" huathiri mitazamo, tabia na nafasi ya mtu katika jamii (Tajfel na Turner, 1979).

Katika muktadha wa vizalia vya watu waliowahi kuchukuliwa utumwani, utambulisho wao huundwa kupitia kumbukumbu jumuishi za kihistoria, ambazo hubeba hisia za pamoja za maumivu, ukombozi na urithi wa pamoja (Sheriff, 1987). Kumbukumbu hizi ambazo mara nyingi huwasilishwa kupitia masimulizi ya kifamilia, fasihi simulizi na mila huchangia katika kuimarisha mshikamano wa kijamii miongoni mwa vizalia. Hata hivyo, kumbukumbu hizo pia huweza kuchochea hisia za kutengwa au unyanyapaa kutoka kwa makundi mengine ya kijamii, hasa pale ambapo historia ya utumwa inahusishwa na unyonge au udhalilishaji wa kihistoria (Deutsch, 2011).

Katika hali kama hiyo, vizalia vya watumwa huweza kukumbana na unyanyapaa wa kijamii, ambapo uhusiano wao na mababu waliowahi kuwa watumwa huonekana kama doa la kijamii. Wakati huohuo, jamii ambazo kihistoria zilihusika kama watekaji au wafanyabiashara wa watumwa huweza kuonekana kwa mtazamo tofauti, hali inayochochea migawanyiko ya kitabaka na kijamii (Nunn, 2008). Migawanyiko hii hujidhihirisha katika lugha, mitazamo ya uraia na nafasi za kijamii, hivyo, kuathiri kwa kiasi kikubwa ujenzi wa utambulisho wa pamoja.

Athari hizi za kihistoria huathiri si tu mitazamo ya kijamii bali afya ya kisaikolojia ya watu binafsi. Branson (2019) anasisitiza kuwa mizigo ya kihisia

inayotokana na historia ya utumwa huweza kuathiri hali ya kujiamini, mahusiano ya kijamii na nafasi ya mtu katika jamii. Katika muktadha huu, Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii hutoa mwanga wa kuchanganua jinsi makovu ya kihistoria yanavyoendelea kuathiri maisha ya sasa, hasa katika uundaji wa utambulisho wa mtu binafsi na wa kijamii.

Zaidi ya hayo, nadharia hii inaweza kuhusishwa na hoja za fasihi na lugha, ambapo simulizi za kihistoria na fasihi simulizi hutumika kama njia ya kuunda na kuendeleza utambulisho wa kijamii. Kama inavyoelezwa na Wodak na wenzake (2009) katika andiko lao la *"The Discursive Construction of National Identity"*, lugha ni chombo cha kuunda maana za kijamii na kitaifa kupitia muktadha. Hii inaendana na hoja za Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii ambayo inasisitiza kwamba binadamu huunda utambulisho wao kupitia simulizi na hujenga utambulisho kwa kuunganisha matukio ya kihistoria katika muktadha wa wakati na maana (Ricoeur, 1991). Kwa hivyo, lugha na fasihi si tu njia za kueleza historia ya utumwa, bali pia ni nyenzo za uponyaji, upinzani na ujenzi wa utambulisho mpya wa vizalia vya watumwa.

Kwa ujumla, Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii inatufundisha kuwa utambulisho wa kijamii si jambo la kudumu au la asili, bali ni zao la mwingiliano wa kihistoria, kijamii na kisaikolojia (Tajfel na Turner, 1979). Katika muktadha wa Tanzania, ambapo kumbukumbu za utumwa bado zina athari, nadharia hii inatoa mwanga wa kuelewa jinsi jamii zinavyounda au kuunda upya utambulisho wao kwa kuzingatia historia ya pamoja, changamoto za sasa na matarajio ya baadaye.

## 4.0 Nadharia ya Kumbukumbu ya Kihistoria na Nadharia ya Fadhaa ya Kizazi

Sehemu hii inajengwa juu ya Nadharia ya Kumbukumbu ya Kihistoria na Nadharia ya Fadhaa ya Kizazi ambazo zinafafanua namna kumbukumbu za utumwa zinavyohifadhiwa na kuendeleza fadhaa ya kihistoria kwa vizalia.

Kumbukumbu ina nafasi muhimu katika kuunda utambulisho na kurithisha fadhaa kwa vizalia (Jedwali 1). Kwa mujibu wa Gross (2015), kumbukumbu inahusisha michakato mitatu ya msingi: usimbaji, uhifadhi na urejeshaji. Matukio ya kikatili kama vile utumwa huacha alama za kihisia kwenye kumbukumbu, hivyo, kuwaathiri watu binafsi na jamii kwa ujumla. Kwa wale waliopitia madhila ya utumwa au ni vizalia vya watu waliowahi kuchukuliwa utumwani, kumbukumbu za udhalilishaji, kuhamishwa kwa nguvu na mateso mara nyingi hudumu na kujidhihirisha katika maisha yao ya kila siku (Gross, 2012).

Utafiti wa Iffland na Neuner (2016) unaonesha kuwa kumbukumbu za fadhaa hutofautiana na kumbukumbu za kawaida kwa kuwa zina athari kubwa zaidi za kihisia. Parry na wenzake (2021) walibainisha kuwa matukio ya fadhaa mara nyingi hujidhihirisha kupitia mawazo ya kinjozi au matukio ya nyuma ambayo huweza kuchangia matatizo ya kisaikolojia kama vile msongo wa mawazo au vurugu za maono.

Katika jamii za Kitanzania zilizoathiriwa na historia ya utumwa, kumbukumbu za fadhaa zimehifadhiwa kupitia masimulizi ya kihistoria, desturi za kitamaduni na kaida za kijamii. Branson (2019) anaeleza kuwa fadhaa inaweza kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, na kuwa na athari kubwa katika afya ya akili ya vizalia. Isobel na wenzake (2021) wanaongeza kuwa fadhaa ya kizazi inaweza kusababisha mabadiliko ya kimuundo katika ubongo, hivyo, kuongeza uwezekano wa matatizo ya afya ya akili.

Athari hizi hazibaki katika kiwango cha mtu binafsi pekee, bali huenea katika familia, jamii na tamaduni kwa ujumla (DeAngelis, 2019). Kwa mfano, Landstedt na Almquist (2019) walionesha kuwa watoto wa wazazi wenye matatizo ya afya ya akili wana uwezekano mkubwa wa kukumbwa na matatizo kama hayo wanapokuwa watu wazima. Zaidi ya hayo, Parra (2023) anasisitiza kuwa fadhaa ambayo haijapatiwa afua inaweza kuendelea kuathiri vizazi vingi vijavyo, na kuathiri mtazamo wao wa maisha, matumaini na uhusiano wao na jamii.

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Athari za Kisaikolojia Zinazotokana na Urithi wa Utumwa katika Jamii za Kitanzania**

| **Kipengele** | **Athari za Kisaikolojia** | **Ufafanuzi** | **Chanzo** |
|---|---|---|---|
| Fadhaa kutokana na utumwa | Hofu, kukosa msaada, mahangaiko | Imesababishwa na uvamizi wa kikatili, misafara ya kulazimishwa, kutengana na familia na udhalilishaji. | Gross (2012) |
| Fadhaa zilizorithishwa kwa vizalia | Mahangaiko ya muda mrefu, msongo wa mawazo, vurugu za maono | Athari za kisaikolojia zinazorithiwa na vizalia, hata bila kuathiriwa moja kwa moja na utumwa. | Branson (2019); Isobel na wenzake (2021) |
| Udhalilishaji | Kiwango cha chini cha kujikubali, fikra dhalili | Ilitokana na kutendewa kama vitu au wanyama, kufanyishwa kazi za kulazimishwa na kuadhibiwa. | DeAngelis (2019) |
| Fadhaa za kiutamaduni | Kupoteza utambulisho, kusahau utamaduni | Watu waliochukuliwa utumwani walinyimwa fursa ya kuishi utamaduni wao, lugha na uhusiano na mababu zao. | Sheriff (1987) |
| Mifumo ya kibaguzi | Kutengwa kijamii, kiuchumi, na kutoshirikishwa | Ubaguzi endelevu wa rangi, mpangilio wa kijamii usio sawa, na tofauti za kiuchumi zinazowakabili vizalia. | Nunn (2008) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kumbukumbu jumuishi | Mahangaiko, vurugu za maono, mgawanyiko wa kijamii | Kumbukumbu za pamoja za fadhaa zinazorithishwa kupitia masimulizi ya kihistoria na msongo endelevu wa kisaikolojia. | Iffland & Neuner (2016) |
| Matatizo ya afya ya akili | Vurugu za maono (PTSD), msongo, mahangaiko | Athari za muda mrefu za fadhaa zinazojidhihirisha baadaye kama matatizo ya kisaikolojia. | Parry na wenzake (2021) |
| Unyanyapaa na mgawanyiko wa kijamii | Mkanganyiko wa utambulisho, udhalili | Unyanyapaa unaohusishwa na ukoo na unaosababisha migawanyiko ya kijamii na kuchochea ubaguzi. | Landstedt na Almquist (2019) |
| Kupoteza uhuru | Kukosa msaada, hasira | Udhalilishaji wa kisaikolojia kutokana na kunyimwa uhuru na kudhibitiwa kwa maisha binafsi. | Gross (2015) |
| Athari za miundombinu ya kihistoria | Kumbukumbu za kale, mahangaiko | Maeneo ya kihistoria kama Bagamoyo na Ujiji huibua kumbukumbu zenye fadhaa kwa jamii zinazozunguka. | Parra (2023) |

### 4.1 Makovu ya Kisaikolojia ya Utumwa Nchini Tanzania

Masalia ya utumwa nchini Tanzania, nchi ambayo ilikuwa kitovu kikuu cha biashara ya utumwa katika Bahari ya Hindi, yameacha makovu makubwa ya kudumu ya kisaikolojia ambayo yanaendelea kuathiri utambulisho na afya ya akili ya mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla (Sheriff, 1987). Ingawa mabaki ya miundombinu ya biashara ya utumwa, kama vile vituo vya biashara, masoko ya watumwa na njia za misafara, ni ukumbusho halisi wa historia hii ya kikatili, athari za kisaikolojia kwa watu waliochukuliwa utumwani na vizalia vyao bado hazijapewa uzito unaostahili katika mijadala ya kijamii na kitaaluma (Deutsch, 2011).

Makovu haya ya kisaikolojia yamekuwa yakirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, na kuunda mtandao changamani wa fadhaa, upotevu wa utambulisho na mapambano ya ndani ya nafsi ambayo yanaendelea hadi leo (Branson, 2019). Vizalia vya watumwa mara nyingi hukumbwa na hali ya mkanganyiko wa utambulisho, hisia za kutengwa, na wakati mwingine, hali ya aibu au unyonge unaotokana na historia ya mababu zao. Hali hii huathiri si tu maisha ya mtu binafsi bali pia mahusiano ya kijamii, nafasi ya kiuchumi na ushiriki wao katika jamii pana.

Zaidi ya hayo, maeneo ya kihistoria kama Bagamoyo, Kilwa na Ujiji ambayo yalihusishwa moja kwa moja na biashara ya utumwa, bado yanabeba kumbukumbu za kihisia kwa jamii zinazozunguka maeneo hayo. Kumbukumbu hizi huweza

kuchochea hisia za huzuni, hasira au hata hofu, hasa pale ambapo historia hiyo haijashughulikiwa ipasavyo kwa njia ya kijamii au kitaasisi (Parra, 2023).

## 5.0 Athari za Fadhaa za Utumwa

Sehemu hii inawasilisha matukio mbalimbali ya kifadhaa yanayotokana na utumwa kwa kurejelea mbinu na taratibu ambazo watumwa walikuwa wanapatikana na kusafirishwa, shughuli muhimu zinazoonesha biashara ya utumwa, mabaki ya miundombinu ya kihistoria na athari za masimulizi ya utumwa yaliyopatikana kwenye matini mbalimbali.

Kwa kawaida, matukio muhimu ya kihisia huacha viashiria vya kumbukumbu thabiti na za kudumu ambazo humsaidia mtu kuyakumbuka kwa miaka mingi baadaye. Iffland na Neuner (2016) wanasisitiza kuwa, ili kuelewa msigano wa kumbukumbu za kifadhaa, ni muhimu kuelewa jinsi kumbukumbu inavyofanya kazi. Hifadhi maalum ya kumbukumbu za matukio ya maisha ya awali hujulikana kama kumbukumbu za episodi (Gross, 2015; Tulving, 2001). Kumbukumbu hizi hujumuisha matukio katika nyakati mahususi na hushughulikia taarifa za kimuktadha kuhusu "nini," "wapi," na "wakati gani" (Iffland na Neuner, 2016).

Kwa hiyo, kumbukumbu za kifadhaa za utumwa zimefumbatwa kwenye episodi za matukio ya watu binafsi. Kumbukumbu ya matukio huruhusu mtu kurejea matukio ya awali kwa uangalifu katika mfumo wa urazini. Hii ina maana kwamba makovu ya kisaikolojia ya utumwa yanaweza yasiwe kumbukumbu tu, bali yanaweza kudhihirika kwa uwazi kama tukio la kuhuzunisha linalojirudia. Matokeo yake, tajiriba hiyo huleta fadhaa ya kisaikolojia miongoni mwa wale waliochukuliwa utumwani na vizalia vyao.

## 5.1 Mchakato wa Kupata Watumwa

Mchakato wa kuwapata watumwa katika maeneo ya Tanzania ya sasa ulikuwa wa kikatili na wa kufadhaisha, na umeacha athari kubwa za kihisia na kisaikolojia kwa waathirika na vizalia vyao. Kwa mujibu wa kumbukumbu za kihistoria, watu wengi walitekwa kwa nguvu kupitia uvamizi wa kijeshi, ambapo vijiji vilivamiwa usiku, nyumba kuchomwa moto na waliopinga au kujaribu kutoroka waliuawa (URT, 1977). Miongoni mwa wahusika wakuu wa uvamizi huu alikuwa Hamad bin Muhammad bin Juma bin Rajab el Murjebi, maarufu kama Tipu Tip, ambaye alihusika moja kwa moja na mashambulizi ya kikatili katika maeneo ya bara ya Tanzania (picha 1), akiteka watu kwa ajili ya biashara ya utumwa (Sheriff, 1987; Glassman, 1995).

Katika misafara mikubwa ya kijeshi aliyoiongoza, Tipu Tip aliteka watu kwa ajili ya biashara ya watumwa na pembe za ndovu. Mateka walilazimishwa kutembea kwa miguu kwa umbali mrefu, wakiwa wamefungwa minyororo mikononi na miguuni huku wakibeba mizigo mizito. Walikumbwa na njaa, magonjwa na ukatili

wa walinzi wao, na wengi walifariki kabla ya kufika pwani (Farrant, 1975; Laing, 2022).

Mbali na uvamizi wa moja kwa moja, njia nyingine ya kupata watumwa ilikuwa kupitia biashara ya moja kwa moja kati ya viongozi wa kijadi na wafanyabiashara wa watumwa. Viongozi wa makabila kama Wayao na Wanyamwezi walihusika katika kuuza watu wao kwa kubadilishana na bidhaa kama bunduki, nguo na chumvi (URT, 1977). Hali hii ilichochea hisia za usaliti miongoni mwa vizalia ambao walihisi kuwa viongozi wao waliwasaliti kwa kushiriki katika biashara hiyo haramu na ya kikatili.




*Picha 1: Mateso waliyopata watumwa*
**Chanzo:** URT (1977)

Zaidi ya hayo, baadhi ya watumwa kutoka Afrika ya Mashariki, wakiwamo waliotoka Tanzania, walisafirishwa hadi maeneo ya Mashariki ya Kati, India, Ulaya na hata Amerika kupitia Bahari ya Atlantiki (tazama Picha Na. 2). Ingawa idadi ya watumwa kutoka Afrika Mashariki ilikuwa ndogo ikilinganishwa na wale waliotoka Afrika Magharibi, njia ya kati (*Middle Passage*) ya safari ya kuvuka Bahari ya Atlantiki ilijulikana kwa ukatili wa hali ya juu. Meli za watumwa zilijaa kupita kiasi, mazingira yalikuwa duni, magonjwa yalienea kwa kasi na walinzi walitumia nguvu kupita kiasi dhidi ya watumwa. Hali hizi zilisababisha athari kubwa za kisaikolojia kwa waathirika, zikiwamo hisia za wasiwasi, mfadhaiko na udhalilishaji wa utu (Mustakeem, 2016; Johnson, 2005).

Kati ya karne ya 16 hadi katikati ya karne ya 19, wafanyabiashara wa Kireno na wa Kibrazili walihusika kwa kiwango kikubwa zaidi katika usafirishaji wa watumwa kupitia Bahari ya Atlantiki. Inakadiriwa kuwa kati ya watumwa milioni 12.5 waliokamatwa kutoka Afrika katika kipindi hicho, zaidi ya milioni 5.8 walisafirishwa kwa meli zilizokuwa chini ya bendera ya Ureno na baadaye Brazili. Wafanyabiashara wa Kiingereza walishika nafasi ya pili kwa kusafirisha karibu watumwa milioni 3.3 ambapo zaidi ya milioni 2.5 kati yao walisafirishwa katika

karne ya 18 pekee ikiwa ni idadi kubwa zaidi ya watumwa waliowahi kusafirishwa na taifa moja katika kipindi cha karne moja (Statista, 2024).



*Picha 2: Watumwa wakisafirishwa kwa meli na kupitia mateso*
**Chanzo:** URT (1977)

Kumbukumbu za matukio ya kikatili ya usafirishaji wa watumwa ziliacha majeraha ya kudumu ya kihisia ambayo yamerithishwa kwa vizalia kupitia masimulizi ya kifamilia, mila na uzoefu wa kijamii. Hali hii imeendeleza hali ya fadhaa ya kihistoria miongoni mwa vizalia, hata baada ya kupita kwa vizazi kadhaa (Ross, 2024; McLaurin, 2025). Tafiti mbalimbali zimebainisha kuwa vizalia vya watumwa hukumbwa na athari za kisaikolojia kama vile msongo wa mawazo, huzuni ya muda mrefu na hisia za kutengwa kijamii (Branson, 2019; Gump, 2017). Mambo haya huongeza mzigo wa kihisia unaorithishwa kizazi hadi kizazi, na kuchochea changamoto zinazohusiana na utambulisho, thamani binafsi na nafasi ya kijamii (Cross, 1998; Bowser na Charles-Nicolas, 2021).

Kwa muktadha huu, mchakato wa kupata na kusafirisha watumwa hauwezi kuonekana tu kama tukio la kihistoria lililopita bali ni chanzo cha maumivu ya muda mrefu yanayoendelea kuathiri maisha ya vizalia vya watumwa nchini Tanzania. Hali hii inasisitiza haja ya kuchunguza kwa kina athari za kihistoria na kuanzisha mikakati ya kijamii na kitaaluma ya uponyaji wa pamoja na ujenzi wa utambulisho chanya kwa jamii zilizoathirika.

### 5.2 Shughuli za Watumwa

Katika kipindi cha biashara ya watumwa Afrika ya Mashariki, watumwa walihusishwa katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo zilikuwa msingi wa ustawi wa jamii za wakati huo. Miongoni mwa shughuli hizo ni pamoja na kazi katika mashamba ya mikarafuu, miwa na mazao mengine ya biashara, hasa katika

maeneo ya pwani na visiwani kama Zanzibar na Pemba. Aidha, baadhi yao walitumika katika uchimbaji wa madini katika maeneo ya bara, wakifanya kazi katika mazingira hatarishi na yenye ukatili mkubwa (Sheriff, 1987; Inikori, 1992).

Watumwa walilazimishwa kufanya kazi kwa saa nyingi bila mapumziko ya kutosha huku wakikumbwa na ukosefu wa chakula bora, huduma za afya na malazi ya heshima. Aidha, walikabiliwa na adhabu kali kwa kosa lolote, ikiwa ni pamoja na kupigwa, kufungwa minyororo, au kunyimwa mahitaji ya msingi (URT, 1977; Hicks, 2015). Mazingira haya ya ukatili na unyanyasaji yaliathiri kwa kiasi kikubwa hali ya kimwili na kisaikolojia ya watumwa.

Hali ya hofu ya kudumu, ukosefu wa udhibiti juu ya maisha yao na mateso ya mara kwa mara vilichochea hali ya huzuni ya muda mrefu, kukata tamaa na hisia za kutokuwa na thamani. Kwa mujibu wa Parry (2021), hali ya hofu ya muda mrefu na kutokuwa na uwezo inaweza kusababisha udhoofu mkubwa wa afya ya akili, jambo lililodhihirika wazi miongoni mwa watumwa waliokuwa wakikumbwa na ukatili wa kila siku.

### 5.3 Mabaki ya Miundombinu na Kiutamaduni


Mabaki ya miundombinu na kiutamaduni ya utumwa nchini Tanzania ni ishara zenye nguvu zinazoendelea kuibua fadhaa na ukinzani. Miji kama vile Bagamoyo, Ujiji, Mikindani na Kilwa vilikuwa vituo vikuu vya biashara na vinatumika kama ukumbusho dhahiri wa udhalilishaji na mateso yaliyotokea (Fouéré, 2015; Lwoga na wenzake, 2024). Maeneo hayo, pamoja na masoko ya watumwa, vituo vya biashara na makaburi, huchochea miitikio ya kihisia kutoka vizalia vya watu waliochukuliwa utumwani. Kwa jamii nyingi zinazoishi karibu na maeneo ya kihistoria, masalia ya utumwa ni urithi na sehemu muhimu ya utambulisho wao wa kijamii na kitamaduni unaoathiri maisha yao ya kila siku kwa kiasi kikubwa. Ama kwa hakika, urithi wa maeneo hayo unabaki katika mfumo wa makumbusho na kumbukumbu ya mateso yaliyotokea. Kwa hiyo, kutembelea sehemu kama hizo kunaweza kusababisha mihemko mikali ikijumuisha huzuni, hasira au hisia ya mwendelezo wa fadhaa za kihistoria.

Kwa mfano, kihistoria, jina Bagamoyo lina maana ya "weka chini moyo wako" (Bwaga Moyo), likimaanisha mwisho wa safari ngumu kwa watu waliochukuliwa utumwani. Watumwa walipofika ufukweni kabla ya kusafirishwa, waliambiwa "waweke chini mioyo yao" kama ishara ya kukubaliana na hatima yao (Sheriff, 1987). Kwa vizalia, maeneo hayo ya kihistoria yanaweza kuibua hisia za maumivu ya mababu, huzuni na hasira, na kuchangia katika kumbukumbu jumuishi ya utumwa ambayo huathiri utambulisho wao. Katika jamii nyingi za Kiafrika, kumbukumbu ya utumwa katika maeneo kama hayo inaendelea kuathiri utambulisho wa kitamaduni na mienendo ya kijamii. Wakati mwingine huimarisha migawanyiko kati ya vikundi vilivyoathiriwa na biashara ya utumwa kwa namna tofauti. Kwa ujumla, hali ya kudumu ya kumbukumbu hizo inaenea zaidi ya nyanja

za kimwili na kijamii na huathiri ustawi wa kihisia na kiakili kwa wale wanaohusika na uwezekano mkubwa kwa vizazi vyote (Alane Hill-Yates, 2012).

Kumbukumbu jumuishi ya utumwa ina jukumu kubwa katika kuunda utambulisho wa jamii mbalimbali, kuathiri jinsi wanavyoainishwa na jinsi wanavyojiona wenyewe leo. Hili hudhihirika zaidi wakati vizalia vya watumwa wanapoungana na mababu zao wa zamani huku wakipitia uhusiano na jamii ambazo zina tajiriba tofauti za kihistoria. Katika muktadha huo, fadhaa ya utumwa huathiri mienendo ya kijamii, mahusiano na utambulisho. Baadhi ya jamii hushikilia hisia kinzani au kustahimili ilhali wengine wanaweza kuhangaishwa na hisia za aibu, kuhamishwa au kupoteza mwendelezo wa kiutamaduni.

Kwa mfano, msafara wa kusini wa biashara ya utumwa ambao ulipitia Kigoma, Tabora na Bagamoyo, unajulikana sana. Wanyamwezi wa Tabora walijulikana kwa uwezo wao wa kubeba mizigo mizito ya pembe za ndovu na bidhaa nyingine hadi ufukweni kupitia njia ya kusini, na kusababisha msemo maarufu wa "mzigo mzito mpe Mnyamwezi" (wapeni Wanyamwezi mzigo mzito) hii inaonesha jukumu la kihistoria na utambulisho wa kitamaduni unaotokana na uzoefu huo (URT, 1997). Mfumo mpya wa mahusiano uliowekwa, uliwaweka watumwa kama watu waliotumikishwa na wanakabiliana na changamoto katika kurudisha urithi wao na kupata nafasi ndani ya jamii ya Kitanzania.




*Picha 3: Njia kuu za biashara ya watumwa Tanzania.*
**Chanzo:** URT (1977)

### 5.4 Simulizi za Utumwa katika Jamii za Watanzania: Ushahidi wa Kihistoria na Kimakavazi


Historia ya utumwa imeandikwa vizuri na inapatikana katika machapisho na makumbusho mbalimbali ndani na nje ya Tanzania. Ingawa mpango huu umefanya kazi nzuri ya kuhifadhi kumbukumbu za kihistoria na kuelimisha vizalia kwa muda

mrefu, pia kuna athari nyingi za kisaikolojia kwa vizalia vya watu waliochukuliwa utumwani. Wakati vizalia wanaposoma katika vitabu, makala au vyanzo vya mitandaoni kuhusu hali halisi ya ukatili wa utumwa, wanaweza kupata mfadhaiko mkali (Fabian, 2013; Rhodes, 2018; Rødland et al., 2020). Fadhaa mbaya hutokea wakati watu huweka ndani maumivu, mateso na mahangaiko ya wengine (Branson, 2019). Ingawa inatokea kwa njia isiyo ya moja kwa moja, inaweza kusababisha changamoto kubwa za mihemuko na kiakili. Kwa mfano, maelezo ya kina kuhusu vurugu, unyanyasaji na utengano wakati wa biashara ya utumwa kupitia Bahari ya Atlantiki inaweza kusababisha hisia za msongo, kutojithamini au hasira kwa wale wenye uhusiano wa kifamilia na historia ya watu waliochukuliwa utumwani. Ingawa ikirari ya historia ya utumwa ni muhimu, mchakato wa kusoma kuhusu historia hiyo unaweza kuwasumbua kisaikolojia vizalia vya baadaye. Zifuatazo ni dondoo na picha kutoka katika vitabu vya kiada vya historia na makala za majarida ambazo zinathibitisha zaidi hoja hii.

> Licha ya kufanya kazi ngumu, watumwa hawakuwa na haki na hawakupokea malipo yoyote kutokana na kazi yao.... Walichapwa viboko, wakakatwa vidole vyao na masikio, na wakati mwingine waliuawa bila sababu yoyote ya maana… Mtumwa angeweza kuamrishwa kupanda juu ya mti mrefu, na kisha Mwarabu akampiga risasi mtumwa huyo. Mwarabu alifurahia kuona mtumwa akianguka na kufa (URT, 1977: 95).

> …kusema ukweli, utumwa ulikuwa wa aibu na mateso. Kwa mfano, mwanamke wa Kiarabu angependa kuona jinsi mtoto anavyolala tumboni basi mjamzito aliweza kukatwa ili mwanamke wa Kiarabu aweze kumwona mtoto ndani (simulizi kutoka kwa Yusuph Samir ambaye alishuhudia utumwa huko Zanzibar iliyonukuliwa na Hill-Yates, 2012: 341)

> Wamiliki wa watumwa wanaweza kukiuka nyanja zote za haki za binadamu ikiwa ni pamoja na kuwabaka. Mke wa mtumwa na binti yake wanaweza kutukanwa mbele ya macho yake bila kuadhibiwa… yeye mwenyewe anaweza kuitwa kuwatesa, na asithubutu kukataa (Patterson, 2024).




*Picha 4: Uvamizi wa kikatili wa kukamata watumwa*
**Chanzo:** URT (1977)

### 5.5 Fadhaa Iliyorithishwa kwa Vizalia

Athari mojawapo kubwa ya kisaikolojia ya utumwa nchini Tanzania ni urithishaji wa fadhaa kwa vizalia. Msongo wa mawazo na udhalili wa kisaikolojia unaosababishwa na utumwa haukuishia na kukomeshwa kwa utumwa; badala yake, ulirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kama Perry na Winfrey (2021) wanavyobainisha kupitia masimulizi:

> Kuelewa jinsi ubongo unavyoitikia msongo au kiwewe cha awali husaidia kufafanua jinsi yaliyotupata zamani yanavyotufanya tuwe tulivyo, jinsi tunavyotenda, na kwa nini tunafanya mambo fulani… (uk. 13).

Kwa kuzingatia kumbukumbu za utumwa, vizalia vya watu waliokuwa watumwa nchini Tanzania wanaendelea kupata madhara ya fadhaa ya kurithi, bila ya kuathiriwa moja kwa moja na ukatili wa utumwa wenyewe. Jambo hili linalojulikana kama fadhaa ya kurithiwa hujidhihirisha katika hali mbalimbali, ikiwa ni pamoja na wasiwasi kupita kiasi, udhalili na kutokuwa na utulivu wa kihisia. Isobel na wenzake (2021) wanaeleza:

> Fadhaa ya kizazi hutokea pale ambapo wazazi waliopitia kiwewe wanapitisha athari za kiwewe chao kwa watoto wao kupitia mwingiliano wa kifamilia, njia za kigeni, au mienendo ya kifamilia ( uk. 632).

Kwa mtazamo wa Kurtz (2018; 2020), hali kama hii inajitokeza katika kile anachokiita mazingira ya kutokeza fadhaa na msongo wa kisaikolojia yaliyosababishwa na biashara ya watumwa, ukoloni na ubaguzi wa kijamii. Anabainisha kuwa jamii kama hizo huendelea "kuishi katika kivuli cha matukio yaliyosambaratisha kumbukumbu, utambulisho na maana ya pamoja" (Kurtz, 2018: 424-425). Hivyo, historia ya utumwa nchini Tanzania ni sehemu ya mfululizo wa

fadhaa na msongo wa kihistoria ambayo imeacha alama za kudumu katika fahamu za vizalia.

Katika utafiti wa Hill-Yates (2012), simulizi za wanawake waliokuwa watumwa zilichanganuliwa ili kubainisha athari za kihisia na kijamii. Simulizi ya Elizabeth Manjadi inaonesha urithishaji wa fadhaa kupitia masimulizi ya kifamilia. Simulizi hii ya kutisha pia inaonesha kiwango cha udhalilishaji wa kibinadamu kilichofanyika na athari zake za kudumu kwa vizalia:

> Bibi yangu aliniambia... wakati wa Kiarabu, mke wa Kiarabu angependa kuona mtu aliyekufa, basi mtumwa aliamriwa kupanda juu ya mnazi na kulazimishwa kuanguka... kama alitaka kuona jinsi mtoto mchanga anavyokuwa kwenye tumbo la uzazi, mwanamke mjamzito anaweza kukatwa ili mke wa Kiarabu aone mtoto. Hayo ndiyo mambo ambayo yananisikitisha sana hadi sasa. Ungejisikiaje kuuawa huku ukiangalia… (uk.341).

Kwa hivyo, simulizi ya Manjadi haipaswi kuonekana tu kama ushuhuda wa kihistoria, bali kama kielelezo cha namna historia ya ukatili inavyoendelea kuathiri maisha ya vizalia. Inatoa mwanga juu ya haja ya mikakati ya kijamii na kitaaluma ya kushughulikia maumivu haya ya kihistoria kwa njia ya maridhiano, uponyaji wa pamoja, na ujenzi wa utambulisho chanya kwa jamii zilizoathirika.

Simulizi nyingine ni ile ya Swema, msichana wa Kiyao kutoka Msumbiji, aliyetekwa kama mtumwa baada ya mama yake kushindwa kulipa deni la mtama. Swema alishuhudia mateso ya mama yake kwenye msafara wa watumwa na baadaye kuzikwa hai na mfanyabiashara wa utumwa wa Kiarabu. Huu ni mfano wa fadhaa ya kurithi. Simulizi ya Swema ni miongoni mwa masimulizi ya awali kabisa yaliyorekodiwa kutoka kwa mateka mmojawapo wa Afrika Mashariki na yaliyonukuliwa na kutafsiriwa na Padre Anthony Horner (Kollman, 2005; Hill, 2012). Baadaye Swema alichukuliwa na wamisionari, akageukia Ukatoliki, akaelimishwa na kuingia katika nyumba ya watawa. Alpers (1983) anaeleza:

> Swema aliuziwa mfanyabiashara wa Kiarabu ili kulipa deni la mama yake. Mama yake alilia na kuomba asitenganishwe na binti yake, lakini kiongozi wa msafara alisisitiza... Swema alichukuliwa na kuanza safari ndefu kuelekea pwani (uk. 191).

Katika simulizi ya Kollman (2005), baada ya Swema kuokolewa na wamisionari wa Kikatoliki na kuelimishwa, hatimaye aliingia katika maisha ya kitawa. Simulizi yake inaonesha si tu athari za awali za jeraha la kisaikolojia bali pia mchakato wa maridhiano wa kihisia unaoashiria kile Kurtz (2018) anachokiita uwezo wa jamii kubadili maumivu kuwa maarifa na msamaha unaohusisha vizalia na watesi wa kihistoria. Swema anasimulia:

> Miaka mingi baadaye, nilikutana na yule Mwarabu aliyenitesa. Nililazimika kumtunza kama muuguzi. Nilimsamehe. Ilikuwa ni mtihani wa imani yangu (Kollman, 2005: 112).

Kwa mujibu wa Kurtz (2018), uponyaji wa fadhaa na msongo wa kisaikolojia unahusisha hatua tatu: kujenga usalama, kukiri hasara na kuunda mahusiano mapya yanayozalisha utambulisho na maana mpya. Kitendo cha Swema cha kumsamehe mtesi wake kinaendana na hatua hii ya mwisho kubadili maumivu kuwa mwelekeo wa maridhiano na imani.

Hadithi ya Swema imerithishwa kwa vizalia vingi miongoni mwa wakazi wa Bagamoyo, hasa ndani ya jumuiya ya watafiti wa Kikatoliki. Inarithishwa kupitia masimulizi ya mdomo na kuhifadhiwa katika kumbukumbu za makumbusho. Hill (2012) anaeleza:

> Simulizi hizi huendelea kuunda kumbukumbu jumuishi ya utumwa vizazi kwa vizazi, zikichagiza utambulisho na mahusiano ya kijamii katika Bagamoyo (uk. 174).

James Mbotela (1956) naye anasimulia fadhaa ya historia ya baba yake, mmoja wa vijana waliokolewa baharini na manowari ya Kiingereza wakati wa harakati za kukomesha biashara ya watumwa katika Bahari ya Hindi. Katika simulizi yake, Mbotela (1956) anaeleza:

> Baba yangu alikuwa mmoja wa vijana waliokolewa baharini na manowari za Waingereza. Alikuwa akisimulia jinsi walivyokuwa wakifungwa minyororo na kusafirishwa kwa mateso (kur.5-15).

Kwa maelezo ya Kurtz (2018: 431), "Ubunifu wa Kiafrika ni mojawapo ya njia kuu za kuunganisha upya kumbukumbu zilizovunjika na kukuza uponyaji wa kijamii." Kwa hivyo, simulizi kama za Swema na James Mbotela (1956) zinatenda kazi kama njia za kijamii za kuponya maumivu ya kihistoria.

Simulizi hizi zinathibitisha kuwa kumbukumbu za mateso na fadhaa ya utumwa zinavyorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Ingawa vizalia havikupitia moja kwa moja ukatili huo, simulizi kama hizi hujenga athari za kihisia na kiutambulisho, zikichochea hisia za huzuni, makovu na maumivu ya kisaikolojia. Aidha, huibua mwelekeo wa maridhiano unaoendana na maono ya Kurtz (2018; 2020) kuhusu uwezo wa jamii za Kiafrika kutumia sanaa na masimulizi kama zana za kubadili fadhaa na msongo wa kisaikolojia kuwa matumaini na maadili mapya ya pamoja. Kwa mtazamo huo, vizalia vya watumwa nchini Tanzania havibebi tu kumbukumbu za maumivu bali pia urithi wa hekima unaoelekeza katika kujenga utambulisho mpya unaotambua maumivu ya zamani huku ukilenga ukombozi na uponyaji wa kiroho na kijamii.

### 5.6 Simulizi kutoka katika Maeneo ya Kihistoria

Utumwa nchini Tanzania haukuathiri tu watu binafsi bali uliacha pia alama ya kudumu katika maeneo kama Bagamoyo, Ujiji na Zanzibar. Maeneo haya yalihusishwa moja kwa moja na biashara ya watumwa na yamehifadhi kumbukumbu za kihistoria kupitia simulizi za mdomo, maandiko na urithi wa kitamaduni. Simulizi hizi zinaonesha jinsi utumwa ulivyokuwa sehemu ya maisha

ya jamii na athari zake za kihisia, kijamii na kiutambulisho ambazo bado zinaonekana hadi leo.

Katika muktadha huu, Bagamoyo ni eneo linalotajwa mara kwa mara katika simulizi za kihistoria kama mahali ambapo watumwa walifikia mwisho wa safari yao kutoka bara. Jina lenyewe linahusishwa na msemo wa kihistoria:

> Watumwa walipofika Bagamoyo, waliambiwa wabwage mioyo yao, maana yake wakubali hatima yao. Hapo ndipo walipokuwa wakisubiri kusafirishwa kwenda Arabuni au India… (Fabian, 2013: 95-114).

Kwa upande mwingine, Ujiji ulikuwa sehemu muhimu ya njia ya watumwa kutoka maeneo ya ndani ya bara kuelekea pwani. Simulizi za wazee na tafiti za kihistoria zinaeleza watumwa waliokamatwa maeneo ya ndani ya bara waliletwa Ujiji, wakafungwa minyororo na kulazimishwa kutembea kwa miguu hadi Bagamoyo. Wengi walikufa njiani kwa njaa, magonjwa na mateso (Becker na Liebst, 2023). Simulizi hizi zinahifadhiwa kupitia miradi ya urithi wa dunia na tafiti zinazolenga kuonesha mateso ya kihistoria na mchakato wa kuondokana na athari zake.

Zanzibar ilikuwa kitovu cha biashara ya watumwa katika Bahari ya Hindi. Simulizi za vizalia na tafiti za kihistoria zinaeleza kwa uchungu kwamba watumwa waliouzwa Zanzibar walihasiwa ili wasizaliane. Wanawake walibakwa au kufanywa masuria. Wengine waliuwawa au kujifia kutokana na mateso (Fouéré, 2020). Fouéré anaeleza kuwa ingawa baadhi ya simulizi kuhusu soko la watumwa Zanzibar zimepotoshwa kihistoria, ukweli kuhusu ukatili wa utumwa na athari zake kwa jamii ya Zanzibar haupingiki. Eneo la soko la zamani la watumwa sasa linahifadhiwa kama sehemu ya urithi wa kihistoria, likiwa na makumbusho na kanisa la Anglikana lililojengwa mahali ambapo watumwa walikuwa wakichapwa na kuuzwa.

Kwa ujumla, masimulizi kupitia fasihi yamekuwa nyenzo kubwa ya kijamii na kihistoria katika kuhifadhi na kuwasilisha kumbukumbu za mateso ya utumwa pamoja na athari zake katika jamii ya Watanzania kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kupitia simulizi zilizorejelewa hapo juu, jamii zimeweza kueleza hisia za makovu, upotevu wa utu, hofu na huzuni ambazo watumwa na vizazi vyao walivipitia, hivyo, kuonesha makovu ya kisaikolojia yaliyosababishwa na utumwa. Masimulizi haya yameendelea kuwa njia ya kukabiliana na kumbukumbu za maumivu kwa kuzigeuza kuwa zana za uponyaji, elimu na kujitambua kwa jamii.

### 5.7 Udhalilishaji na Udhalili wa Kisaikolojia

Utumwa uliwadhalilisha watu kwa utaratibu mahususi na kutweza utu wao ili kuwafanya wajione kama bidhaa inayoweza kununuliwa, kuuzwa na kunyonywa. Upotevu huu mkubwa wa utu na heshima uliacha makovu makubwa ya kisaikolojia. Watu waliokuwa watumwa walionekana kama bidhaa, walifanyiwa vurugu za kila aina, walilazimishwa kufanya kazi ngumu na kupokonywa ubinadamu wao (Davis, 2006; Mapunda, 2017; Al-Kadery, 2024). Patterson (2024) anaongeza kuwa ulimwenguni kote watumwa walichukuliwa kuwa ni watu wasiostahili heshima,

hivyo, kusababisha utwezaji mkubwa wa utu. Walitendewa kama watu ambao wameshakufa kijamii. Udhalili wa kisaikolojia ulisababisha msongo wa mawazo wa muda mrefu, na udhalili na hisia za kukosa thamani (Longman-Mills, 2016; Jackson na wenzake, 2018). Kwa vizalia wengi, hisia hizo za kudunisha utu zimeendelea na kuchangia katika mapambano yanayoendelea ya kujistahi na kujitambulisha. Makovu ya kihisia ya kutendewa kama watu duni yanaendelea kuathiri jamii za Kitanzania, ambapo vizazi vya watu waliochukuliwa utumwani mara nyingi hukabiliana na unyanyapaa wa kijamii na kubaguliwa.

### 5.8 Fadhaa ya Kiutamaduni na Upotevu wa Utambulisho

Makovu ya kisaikolojia ya utumwa nchini Tanzania pia yanahusishwa sana na fadhaa ya kiutamaduni na upotevu wa utambulisho. Utumwa kwa asili yake ulihusisha kumtenga mtu na ulimwengu wa kijamii ambamo amezaliwa (Alane Hill-Yates, 2012). Kwa hiyo, watu waliokuwa watumwa waliondolewa kwa nguvu kutoka katika nchi zao, waliondolewa tamaduni zao na mara nyingi walikatazwa kudumisha uhusiano na wahenga wa jamii zao. Fadhaa hii ya kiutamaduni imekuwa na athari za kudumu kwa vizalia wao wanaoendelea kupambana na hisia za kutengwa na mizizi ya utamaduni wao. Kupotea kwa lugha, mila na desturi za kiimani kumezua hali ya kupoteza kumbukumbu ya kitamaduni, ikichanganya na makovu ya kisaikolojia ya utumwa (Perry, 2023).

Ama kwa hakika, wakati wafanyabiashara ya utumwa walipowateka wanaume na wanawake wenye nguvu za kimwili, waliwaacha wazee, walemavu na waliopo kwenye mazingira hatarishi na kukosa usalama (Ewald, 2017). Waliwafanya waathirike na unyonyaji, vurugu au kutelekezwa. Hii ina maana kwamba madhara ya utumwa yalikuwa zaidi ya unyonyaji wa kimwili kwani ulisababisha pia mgawanyiko mkubwa wa kiutamaduni na kihisia (Marshall na Kiriama, 2018; Patterson, 2024). Watu waliochukuliwa utumwani waliondolewa uasili wao, na hivyo kusababisha si tu kupoteza utambulisho bali kuunda pia utambulisho mpya ndani ya majukumu yao mapya (Mbilinyi, 1988). Mahusiano mapya yaliwafanya watumwa kuwa tegemezi na kuwa watii ndani ya mifumo ya kijamii ya wamiliki wao. Fadhaa hii ya kiutamaduni inadhihirika hasa katika jamii ambazo vizalia vya watu waliochukuliwa utumwani hukabiliana na changamoto katika kurejesha urithi wao na kuendesha nafasi zao ndani ya jamii ya Kitanzania.

### 5.9 Madhila ya Kimfumo na Ubaguzi wa Rangi

Hata baada ya kukomeshwa rasmi kwa utumwa, makovu ya kisaikolojia ya biashara hiyo yaliendelezwa kupitia madhila ya kimfumo na ubaguzi wa rangi (Gill, 2021). Mifumo ya unyonyaji na ubaguzi iliyoanzishwa wakati wa biashara ya utumwa iliendelea na kuimarisha matabaka ya kijamii ambayo yaliwanyima fursa wazawa wa watu waliochukuliwa utumwani (Gwajima na Elizabeth, 2018). Jamii hizo mara nyingi zilikabiliwa na matatizo ya kiuchumi, kutengwa na jamii na ubaguzi wa rangi; yote hayo yalizidisha fadhaa za kisaikolojia kutokana na tajiriba zao za

kihistoria (O'Neil, 2009). Madhila ya utumwa na ubaguzi wa rangi yamefungamana na mifumo isiyo na usawa inayoendeleza fadhaa zinazozikumba jamii za Kitanzania. Tanzania Bara, athari za kihistoria za utumwa bado zinajitokeza kupitia urithi wa kijamii na kiutambulisho, ingawa ushahidi wa ubaguzi wa rangi wa moja kwa moja katika hali ya sasa ni mdogo (Mullings, 2005; Hill, 2012). Tafiti za urithi wa utumwa katika maeneo kama Bagamoyo na Mikindani zinaonesha kuwa vizalia vya watumwa hukabiliana na changamoto za kijamii na hisia za kutengwa, hasa katika muktadha wa urithi wa kihistoria na kumbukumbu za utumwa (Hill, 2012; Lwoga na wenzake, 2024). Hali hii huathiri namna wanavyojiona na nafasi zao katika jamii, na kwa baadhi ya familia, urithi wa kihistoria umechangia upungufu wa rasilimali na fursa za kijamii, ingawa tafiti za kina kuhusu hali ya kiuchumi ya sasa bado zinahitajika.

Ukosefu wa fursa za kiuchumi hudumisha duara la umaskini na msongo wa kisaikolojia (O'Neil, 2009; Hill, 2012; Gwajima na Elizabeth, 2018). Kadhalika, huko Zanzibar, urithi wa utawala wa Waarabu na mivutano ya rangi iliyofuata vimesababisha madhila na ubaguzi wa mara kwa mara. Mienendo ya kisiasa na kijamii Zanzibar imeathiriwa sana na migawanyiko ya kihistoria, huku utambulisho wa rangi na kabila ukiwa na nafasi kubwa katika migogoro ya sasa (Sulley, 2013). Sulley (2013) anaeleza kuwa vurugu za uchaguzi na migawanyiko ya kisiasa Zanzibar zinatokana na historia ya mapinduzi ya 1964 na urithi wa utawala wa Waarabu, hali inayofanya utambulisho wa kikabila na rangi kuwa kiini cha mvutano wa kisiasa. Mivutano hii ni mwendelezo wa moja kwa moja wa madhila ya kimfumo yaliyoanzishwa wakati wa enzi ya biashara ya utumwa.

## 6.0 Mbinu za Kukabiliana na Kustahimili Urithi wa Utumwa

Katika muktadha wa Tanzania ya leo, uwekaji wa kumbukumbu, uanzishwaji wa makumbusho, na sherehe za kiutamaduni zenye historia ya utumwa zimekuwa sehemu muhimu ya mchakato wa uponyaji wa kihistoria. Maeneo kama Bagamoyo, Kilwa, Mikindani na Ujiji yameibuka kama vituo vya kumbukumbu ya maumivu ya utumwa, ambapo jamii hukusanyika kwa ajili ya kutafakari, kuomboleza, na kujifunza kutokana na historia hiyo chungu (Lwoga na Adu-Ampong, 2020; Gill, 2021; Rhodes, 2018). Majukwaa haya yamechochea majadiliano kuhusu maridhiano ya kihistoria na kutoa nafasi ya uponyaji wa pamoja kwa jamii zilizoathiriwa.

Mbali na makumbusho na maeneo ya kihistoria, masimulizi ya kimapokeo yameendelea kuwa njia muhimu ya kutunza kumbukumbu hizo. Masimulizi haya, yanayopitishwa kutoka kizazi hadi kizazi kwa njia ya mdomo, huchukua nafasi ya maandiko rasmi katika kuhifadhi historia ya utumwa. Yamekuwa si tu njia ya kuendeleza kumbukumbu, bali pia zana ya uponyaji wa kihisia, kwa kuwawezesha vizalia kueleza maumivu yao, kuelewa historia yao na kujenga utambulisho wa pamoja. Kwa mujibu wa Sheriff (1987) na Marshall (2021), masimulizi haya

huchangia katika kuimarisha mshikamano wa kijamii na kuendeleza dhamira ya kustahimili licha ya maumivu ya kihistoria.

Kwa pamoja, juhudi hizi za uwekaji wa kumbukumbu, makumbusho, sherehe za kiutamaduni na masimulizi ya mdomo zinatoa njia mbadala kwa jamii ya Kitanzania kukabiliana na ukweli wa maisha yake ya kihistoria. Zinajenga afua endelevu za uponyaji wa kisaikolojia, kuimarisha utambulisho wa pamoja na kuchochea mchakato wa maridhiano ya kihistoria unaohitajika kwa ustawi wa jamii kwa ujumla.

## 7.0 Hitimisho

Makovu ya kisaikolojia yaliyoachwa na utumwa nchini Tanzania ni makubwa na changamani, yakiathiri mtu binafsi na jamii kwa ujumla hata muda mrefu baada ya kukomeshwa kwa biashara ya utumwa. Simulizi mbalimbali zimeonesha kuwa fadhaa za kihistoria, kazi za kulazimishwa, na kutengwa kijamii zimerithishwa kwa vizalia na kudhihirika katika masuala ya afya ya akili na mienendo ya kijamii. Hata hivyo, jamii za Kitanzania zimeonesha ustahimilivu mkubwa kwa kutumia masimulizi ya kimapokeo, mila na tamaduni, pamoja na imani za kidini kama njia za kukabiliana na madhila ya kihistoria. Mbinu hizi zimekuwa msingi wa kujenga mchakato wa uponyaji wa pamoja, kuimarisha utambulisho wa kijamii na kuendeleza majadiliano ya maridhiano.

Makala hii imeangazia umuhimu wa kuendeleza tafiti kuhusu athari za kisaikolojia za utumwa katika Afrika Mashariki, hususani Tanzania, na kuhimiza kuungwa mkono kwa mipango inayokuza uponyaji wa kihistoria kupitia fasihi, sanaa na makumbusho. Kwa kukuza uelewa wa masuala haya, Tanzania inaweza kuendelea kushughulikia majeraha ya kihistoria ya utumwa na kuchangia katika ujenzi wa jamii jumuishi zaidi, yenye ustawi wa kisaikolojia na inayothamini haki za binadamu na utu wa kila mmoja. Kwa kutumia Nadharia ya Utambulisho wa Kijamii, Nadharia ya Kumbukumbu ya Kihistoria na Nadharia ya Fadhaa ya Kizazi, makala hii imeonesha kuwa makovu ya utumwa si kumbukumbu za zamani pekee bali ni urithi hai unaoathiri vizalia na jamii ya Tanzania ya leo.

## Marejeleo


Alane Hill-Yates, E. (2012). “What's in a Tale? Slavery, Memory and the Intersections of Race, Class and Gender in Coastal Tanzania”. *Race, Gender and Class*. 19(2): 336-352.

Al-Kadery, S.A. (2024). “Slavery as a Cultural Legacy: Abdulrazzak Gurnah’s Paradise as a Case Study”. *Arab World English Journal for Translation and Literary Studies*. 8(4): 11-19. http://dx.doi.org/10.24093/awejtls/vol8no4.2

Alpers, E.A. (1975). *Ivory and Slaves in East Central Africa: Changing Patterns of International Trade in East Central Africa to the Later Nineteenth Century*. University of California Press. https://doi.org/10.1525/9780520312197.

Banshchikova, A. na Ivanchenko, O.V. (2019). "Historical Memory of the 19th-century Arab Slave Trade in Modern-day Tanzania: Between Family Trauma and State-planted Tolerance". Katika D.M. Bondarenko na M.L. Butovskaya (Wah.), *The Omnipresent Past: Historical Anthropology of Africa and African Diaspora*. Moscow: LRC Publishing House. Kur. 23-45 https://www.anthropos.eu/anthropos/journal/abstracts/1182/118-2-08.php

Becker, F. (2021). "Looking for Life: Traces of Slavery in the Structures and Social Lives of Southern Swahili Towns". *Journal of African Diaspora Archaeology and Heritage*. 10(1-2): 87-109.

Becker, F., Nyanto, S. S., Giblin, J., McDougall, A., Meckelburg, A., na Pelckmans, L. (2023). "Researching the Aftermath of Slavery in Mainland East Africa: Methodological, Ethical, and Practical Challenges". *Slavery and Abolition*. 44(1): 131–156. https://doi.org/10.1080/0144039X.2022.2121888

Bowser, B. P. na Charles-Nicolas, A. (Wah.). (2021). *The Psychological Legacy of Slavery: Essays on Trauma, Healing and the Living Past*. McFarland, M03 23-307 https://books.google.com/books/about/The_Psychological_Legacy_of_Slavery.html?id=gPclEAAAQBAJ

Branson, D.C. (2019). "Vicarious Trauma, Themes in Research, and Terminology: A Review of Literature". *Traumatology*. 25(1): 2–10. https://doi.org/10.1037/trm0000161.

Cross, W.E.Jr. (1998). "Black Psychological Functioning and the Legacy of Slavery: Myths and Realities". Katika Y. Danieli (Mh.), *International Handbook of Multigenerational Legacies of Trauma*. Plenum, New YorkKur.387-400. https://doi.org/10.1007/978-1-4757-5567-1_25

Curtin, P.D. (1969). *The Atlantic slave trade: A census*. Madison: University of Wisconsin Press.

Davis, D.B. (2006). *Inhuman Bondage: The Rise and Fall of Slavery in the New World*. New York. Oxford University Press.

DeAngelis, T. (2019). "The Legacy of Trauma: An Emerging Line of Research is Exploring how Historical and Cultural Traumas Affect Survivors' Children for Generations to Come". *Monitor on Psychology*. Kur. 36, 50(2). https://www.apa.org/monitor/2019/02/legacy-trauma.

Deutsch, J.G. (2011). "Memory, Oral History and the End of Slavery in Tanzania: Some Methodological Considerations". Katika P. Lane na K. MacDonald (Wah.), *Slavery in Africa: Archaeology and Memory*. Oxford: Oxford University Press. Kur. 187-204.

Deutsch, J.G. (2006). *Emancipation without Abolition in German East Africa, c. 1884–1914*.Oxford: James Currey. https://doi.org/10.3366/E0001972008260274

Deutsch, M. (2011). "Stigma and Social Identity". In T.L. Anderson (Mh.), *Understanding Deviance: Connecting Classical and Contemporary Perspectives* New York. Routledge. Kur. 256-265.

Ewald, J.J. (2017). "Slavery in Africa and the Slave Trades from Africa". Katika J. Black (Mh.), *The Atlantic Slave Trade*. London: Routledge. Kur. 119-139. https://doi.org/10.4324/9781351147682.

Fabian, S. (2013). East Africa's Gorée: Slave Trade and Slave Tourism in Bagamoyo, Tanzania. *Canadian Journal of African Studies/La Revue Canadienne des Études Africaines*. 47(1): 95-114.

Farrant, L. (1975). *Tippu Tip and the East African Slave Trade*. London: Hamish Hamilton. Available online.

Fouéré, M.A. (2020). "Museumizing the Slave Trade and Slavery in Zanzibar: Truth, Untruth, and Uncertainty at the Old Slave Market". *Ethnologie Française.* 50(1): 109-124. https://doi.org/10.3917/ethn.201.0109.

Fouéré, M.A. na Hughes, L. (2015). "Heritage and Memory in East Africa Today: a Review of Recent Developments in Cultural Heritage Research and Memory Studies". *Azania: Archaeological Research in Africa*. 50(4): 542-558.

Gill, S. (2021). *Healing the Wounds of Slavery: A Conceptual Framework*, Brighton: Guerrand-Hermes Foundation for Peace.

Glassman, J. (1995). "The Bondsman's New Clothes: The Contradictory Consciousness of Slave Resistance on the Swahili Coast". *The Journal of African History*. 36(2): 277-312. https://doi.org/10.1017/S0021853700034263.

Gross, J.J. (2012). "Emotion Regulation: Affect, Cognitive, and Social Consequences". *Psychophysiology.* 39(3): 281-291. https://doi.org/10.1017/S0048577201393198.

Gross, J.J. (2015). "Emotion Regulation: Current Status and Future Rospects". *Psychological Inquiry*. 26(1): 1-26. https://doi.org/10.1080/1047840X.2014.940781.

Gross, R. (2012). *Psychology: The Science of Mind and Behaviour*. 6th Edition: London. Hodder Education.

Gump, J.P. (2017). "The Study of Trauma: A Historical Overview". Katika S.N. Gold (Mh.), *APA Handbook of Trauma Psychology:* Juz. 1*: Foundations in Knowledge* (1–11). https://doi.org/10.1037/0000019-001.

Gwajima, S. na Elizabeth, K. (2018). "The Representation of Structural Violence in *Makuadi wa Soko Huria* (*The Free Market Pimps*)". *Tanzania Zamani.* 10(1): 144-179.

Heywood, L.M. (2003). "Recreating Africa: Culture, Kinship, and Religion in the African-Portuguese World, 1441-1770". *The International Journal of African Historical Studies.* 36(3): 693-694.

Hicks, S. R. (2015). *A critical Analysis of Post Traumatic Slave Syndrome: A Multigenerational Legacy of Slavery*. San Francisco: California Institute of Integral Studies.

Hill, E. (2012). *Bearing the Mark, Bearing the Costs: Memories of Slavery in Coastal Tanzania, 1922–2008.* Tasnifu ya Uzamivu Isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Illinois, Urbana-Champaign. https://hdl.handle.net/2142/31938.

Iffland, B. na Neuner, F. (2016). "Trauma and Memory". Katika G. Fink (Mh.), *Stress: Concepts, Cognition, Emotion, and Behavior.* London. Academic Press. Kur. 161-167. https://psycnet.apa.org/record/2016-26280-019.

Inikori, J.E. (1992). "Africa in World History: the Export Slave Trade from Africa and the Emergence of the Atlantic Economic Order". *General History of Africa*. 5: 74-112.

Isobel, S., McCloughen, A., Goodyear, M., na Foster, K. (2021). "Intergenerational Trauma and its Relationship to Mental Health Care: A Qualitative Inquiry". *Community Mental Health Journal*. 57(4): 631-643. https://doi.org/10.1007/s10597-020-00698-1.

Jackson, L., Jackson, Z., na Jackson, F. (2018). "Intergenerational Resilience in Response to the Stress and Trauma of Enslavement and Chronic Exposure to Institutionalized Racism". *Journal of Clinical Epigenetics*. 4(3). 15.

Johnson, M.V. (2005). "The Middle Passage, Trauma and the Tragic Re-Imagination of African American Theology". *Pastoral Psychology*. 53(6): 559-570. https://doi.org/10.1007/s11089-005-4820-4.

Katz, W.L. (2024). *Breaking the Chains: African American Slave Resistance*. Lost Horses: Seven Stories

Kollman, P.V. 2005. *The Evangelization of Slaves and Catholic Origins in Eastern Africa*. Maryknoll, NY: Orbis Books.

Kurtz, J.R. (Ed.). (2018). *Trauma and Literature*. Cambridge: Cambridge University Press. https://doi.org/10.1017/9781316817155

Kurtz, J. R. (2020). *Trauma and Transformation in African Literature (*1st ed.). Routledge. https://doi.org/10.4324/9781315467535

Laing, A. (2022). *The Legacy of Slavery in Coastal Kenya: Memory, Identity, and Heritage*. Lanham, MD. Rowman & Littlefield. Review & summary

Landstedt, E. na Almquist, Y.B. (2019). "Intergenerational Patterns of Mental Health Problems: The Role of Childhood Peer Status Position". *BMC Psychiatry*. 19, Article 286. https://doi.org/10.1186/s12888-019-2278-1

Longman-Mills, S., Mitchell, C., na Abel, W. (2019). "The Psychological Trauma of Slavery: The Jamaican Case Study". *Social and Economic Studies*. 1: 79-101.

Lovejoy, P.E. (2012). *Transformations in Slavery: A History of Slavery in Africa* (3rd ed.). Cambridge. Cambridge University Press. https://doi.org/10.1017/CBO9781139014946

Lwoga, N.B.; Adu-Ampong, E.A. (2021) "Heritage and Heritage Tourism in Africa: Historical Overview and Contemporary Issues". Katika Novelli, M., Adu-

Ampong, A.A., Ribeiro, A., (Wah.), *Routledge Handbook of Tourism in Africa*. London: Routledge: Kur. 69-84.

Lwoga, N. B., Chami, M., Kafumu, B., Kisusi, R., & Ndahani, P. (2024). "Multivocality and its implications for the representation of heritage: A case study of the slavery heritage in Mikindani, Tanzania". *Journal of Heritage Management, 9*(1), 52–72. New Delhi. SAGE https://doi.org/10.1177/24559296241249242.

Mapunda, B.B. (2017). "Encounter with an "Injured Buffalo:" Slavery and Colonial Emancipation in Tanzania". *Journal of African Diaspora Archaeology and Heritage*. 6(1): 1-18.

Marshall, J. (2021). *(Im) mobility in a Sea of Migration: Race, Mobilities, and Transnational Families in Zanzibar and Oman, 1856-2019*. Michigan: Michigan State University.

Marshall, L.W. na Kiriama, H. (2018). "The Legacy of Slavery on the Swahili Coast." Katika S. Wynne-Jones na A. LaViolette (Wah.), *The Swahili World* London: Routledge. Kur. 566-576.

Mason, J.E. (2002). "A Faith for Ourselves': Slavery, Sufism, and Conversion to Islam at the Cape". *South African Historical Journal*. 46(1): 3-24.

Mbilinyi, M. (1988). "Agribusiness and Women Peasants in Tanzania". *Development and Change*. 19(4): 549-583.

Mbotela, J. (1956). *The Freeing of the Slaves in East Africa*. London: Evans Brothers Ltd. https://books.google.co.tz/books?id=uAzTAAAAMAAJ&source=gbs_book_other_versions

McEwen, M. (2018). *Spaces Surrounding Freedom: Enslaved Women's Resistance and Agency on the East Coast of Africa in the 1890s*. (Tasnifu ya Shahada Uzamivu isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Jimbo la New York (The State University), Buffalo.

McLaurin, C.W. (2025). *A Phenomenological Study of Intergenerational Trauma of African Americans in the South and Post Traumatic Slave Syndrome*. Liberty University. https://digitalcommons.liberty.edu/doctoral/7293.

Mikidady, M. (2023). "A History of Slave Trade in Northeastern Tanzania: A Case of Bondei People, 1800-1900". *Journal of African History and Archaeology*. 1(1): 9-24.

Mullings, L. (2005). "Interrogating Racism: Toward an Antiracist Anthropology". *Annual Review Anthropology*. 34: 667-693. https://doi.org/10.1146/annurev.anthro.32.061002.093435.

Mustakeem, S. M. (2016). *Slavery at Sea: Terror, Sex, and Sickness in the Middle Passage*. Urbana. University of Illinois Press. https://doi.org/10.5406/illinois/9780252040559.003.0006.

Nunn, N. (2008). "The long-term effects of Africa's Slave Trades". *The Quarterly Journal of Economics*. 123(1): 139-176. https://doi.org/10.1162/qjec.2008.123.1.139.

Nunn, N. (2017). "Understanding the Long-run Effects of Africas Slave Trades". *The Long Economic and Political Shadow of History*, 2: 36-48.

Nyanto, S.S. na Becker, F. M. (2025). "Kijiji cha Watoro: Resistance, Identity, and Social Life of Nyamwezi Runaway Slaves along the Central Caravan Route in Tanzania". *Slavery & Abolition*. 46(3): 567-586. https://doi.org/10.1080/0144039X.2025.2532901.

O'Neil, E. (2009). "Poverty, Structural Violence, and Racism in a World out of Balance". *Race/Ethnicity: Multidisciplinary Global Contexts*. 3(1): 115-138.

Parra, C. (2023). "Breaking the Chains of Generational Trauma". *Sociology Student Work Collection*, 90. University of Washington Tacoma. https://digitalcommons.tacoma.uw.edu/gender_studies/90.

Parry, J.A., Kang, K.K., Ciminero, M.L. na Mauffrey, C. (2021). "The Psychological Effects of Musculoskeletal Trauma". *Journal of the American Academy of Orthopaedic Surgeons*. 29(7): e322–e329. https://doi.org/10.5435/JAAOS-D-20-00637.

Parry, T.D. (2021). "How Much More Must I suffer?: Post-traumatic Stress and the Lingering Impact of Violence upon Enslaved People". *Slavery & Abolition*. 42(2): 184-200. London. Taylor & Francis.

Patterson, O. (2018). *Slavery and Social Death: A Comparative Study, with a New Preface*. Harvard: Harvard University Press.

Paul, S. A. (2009). *The Ubuntu God: Deconstructing a South African Narrative of Oppression.* Eugene: Wipf and Stock Publishers.

Perry, V. L. (2023). *African Traditional Healing Through Spirituality: An Alternative Treatment for Transgenerational Trauma in the African American Community* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Howard, Washington, DC.

Rhodes, D. T. (2018). "History, Materialization, and Presentation of Slavery in Tanzania". *Journal of African Diaspora Archaeology and Heritage*. 7(2): 165-191. London. Taylor & Francis. https://doi.org/10.1080/21619441.2019.1589714.

Ricoeur, P. (1991). "Narrative identity". *Philosophy Today.* 35(1): 73-81. Chicago: Philosophy Documentation Center. https://doi.org/10.5840/philtoday199135136.

Rødland, H., Wynne-Jones, S., Wood, M., na Fleisher, J. (2020). "No such thing as Invisible People: Toward an Archaeology of Slavery at the Fifteenth-century Swahili site of Songo Mnara". *Azania: Archaeological Research in Africa*. 55(4): 439-457.

Ross, C.C. (2024). "Slavery and race-based trauma: The impact of historical and intergenerational trauma on health". Katika N. Kim et al. (Wah.), *Antiblackness and the stories of authentic allies: Lived experiences in the fight against institutionalized racism* (uk. 25–44). New York. Oxford University Press**.** https://doi.org/10.1093/oso/9780197642535.003.0002.

Rushohora, N. (2024). "Memories of Resistance to Slavery in South-eastern Tanzania". *Journal of Humanities and Social Sciences*,.13(2): 57-69. https://doi.org/10.56279/13/2/3.

Sheriff, A. (1987). *Slaves, Spices and Ivory in Zanzibar: Integration of an East African Commercial Empire into the World Economy, 1770–1873*. Woodbridge. Boydell & Brewer. https://doi.org/10.1515/9781782049784

Statista. (2024). "African Slaves Taken by Each Nation 1501–1866". Retrieved from https://www.statista.com/statistics/1150477/number-slaves-taken-by-national-carriers/

Sulley, C.R. (2013). Electoral Violence in Africa: A Comparative Analysis of Kenya and Tanzania. *The African Review*. 40(2): 80-114.

Sunseri, T. (2002). *Vilimani: Labor Migration and Rural Change in Early Colonial Tanzania*. Portsmouth, NH: Heinemann.

Tajfel, H., na Turner, J.C. (1979). "An Integrative Theory of Intergroup Conflict". Katika W.G. Austin na S. Worchel (Wah.), *The Social Psychology of Intergroup Relations*. Monterey, CA: Brooks/Cole. Kur. 33-47.

Tulving, E. (2001). "Episodic Memory and Sommon Sense: How Far Apart?" *Philosophical Transactions of the Royal Society of London. Series B: Biological Sciences*. 356(1413): 1505-1515.

United Republic of Tanzania (URT). (1977). *Historia ya Tanzania Kabla ya 1880*. Dar es Salaam. Government Printer.

Wodak, R., de Cillia, R., Reisigl, M., na Liebhart, K. (2009). *The Discursive Construction of National Identity* (2nd Ed.). Edinburgh: Edinburgh University Press.

Wright, M. (1993). *Strategies of Slaves and Women: Life-stories from East/Central Africa*. New York: Lillian Barber Press; London: James Currey. urn:oclc:record:984681833